

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, SACP Wilbroad Mutafungwa (kulia), akionyesha kwa waandishi wa habari, mkoani humo jana, baadhi ya vifaa vya uvuvi vinavyodaiwa kuwa ni vya wizi zikiwamo nyavu za uvuvi haramu aina ya kokolo vilivyokamatwa katika msako wa wiki moja uliofanywa na jeshi hilo. **PICHA: VITUS AUDAX**

NIPASHE UKID.

# Jeshi la Polisi lakamata shehena ya vifaa vinavyotumika kwa uvuvi haramu

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza limekamata shehena ya vifaa vya uvuvi vinavyosadikiwa kuwa vya wizi pamoja na vingine vinavyotumika katika uvuvi kinyume cha sheria.

Vitu vilivyokamatwa ni pamoja na mashine za boti 12, mitumbwi 18 iliyokutwa na nyavu 1,202, mitumbwi minne isiyokuwa na namba za usajili kinyume cha sheria ambayo pia ilikutwa na nyavu haramu 10.

Akitoa taarifa hiyo juzi kwa waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, SACP Wilbroad Mutafungwa, alisema miongoni mwa nyavu 1,202 zilizokamatwa na jeshi hilo 387 zimetambuliwa na watu walioibiwa.

Vilevile alisema kuwa katika mikutano ya hadhara waliyoifanya katika maeneo mbalimbali mkoani Mwanza walibaini uwepo wa kero ya vitendo vya wavuvi kuvamiwa nyakati za usiku na kunyang'anywa mali zao.

"Katika msako huo kupitia polisi wetu pamoja na idara ya uvuvi mkoani hapa tumefanikiwa kuwakamata watu watano wanaotuhumiwa kuhusika na uvamizi huo katika maeneo mbalimbali ya visiwa vya Ziwa Victoria," alisema SACP Mutafungwa.

Kadhalika, alisema baadhi ya wavuvi waliokuwa wakitumia nyavu zilizokamatwa walizikimbia hali inayoashiria kuwa walikuwa wakizitumia kinyume na sheria.

Alisema operesheni hiyo endelevu ilianza Septemba 26 ikifanyika katika maeneo ya visiwa vya Bezi, Ikulu, Ito, Ntama na kwenye mialo mingine sita iliyopo katika Halmashauri ya Ilemela pamoja na Nyamagana.

Naye Ofisa Mfawidhi wa Ulinzi na Usimamizi wa Rasilimali za Uvivi Kanda ya Ziwa Victoria, Farah Bulongo, aliwataka wavuvi wote kufanya uvuvi wenye tija ili kuhakikisha sekta ya uvuvi inakuwa endelevu na kuacha matumizi ya zana haramu.

CamScanner

iliyofanyika Mgodi wa North ...
Tarime Vijijini, Mwita Waitara. (Picha kwa hisani ya Barrick).

HABARI LEO UK 14.




Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (katikati) akipokea zawadi kutoka kwa Balozi wa Uholanzi nchini, Wiebe de Boer kwenye warsha ya siku moja kuhusu umuhimu wa kuongeza ushindani kwenye sekta ya vyakula vya mifugo vyenye protini iliyoandaliwa na ubalozi huo kwa kushirikiana na Mpango wa Kukuza Kilimo Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) mkoani Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kutoka kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa SACGOT, Geoffrey Kirenga na Mkurugenzi wa Ufugaji wa Samaki wa wizara hiyo, Dk Nazaeli Madalla (wa pili kulia). (Na Mpigapicha Wetu).

MWANANCHI UK 3.

# Ng'ombe wa Rais Samia waponza watatu

**Mgongo Kaitira**, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Mwanza.** Watu watatu, akiwemo mfanyakazi wa shamba la mifugo la Mabuki lililoko Wilaya ya Misungwi, mkoani Mwanza wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa mahojiano kuhusu madai ya kuhusika na upotevu wa ng'ombe sita katika shamba hilo.

Ng'ombe waliopotea ni kati ya 600 waliotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa shamba hilo kwa ajili ya kituo atamizi katika Ranchi ya Mabuki kwa lengo la kunufaisha vijana kupitia mradi wa "Jenga Kesho Iliyobora", maarufu kama (BBT).

Bila kutaja majina ya watuhumiwa wanaoshikiliwa, Mkuu wa Wilaya ya Misungwi, Paulo Chacha alisema msako wa kutafuta ng'ombe waliopotea unaendelea.

"Tayari ng'ombe wanne wamepatikana na kurejeshwa, huku juhudi zaidi zikiendelea kuwasaka ng'ombe wawili waliosalia," alisema Chacha, aliyezungumza na *Mwananchi* kwa njia ya simu jana.

Alisema kabla ya kubaini upotevu huo, Serikali ilipata taarifa ya kuwepo mchezo wa kutoweka kwa mifugo kwenye shamba hilo na wanaendelea kusaka mtandao wa wizi.

"Tulibaini kuwepo mchezo, tukaweka mtego, Jumapili tukabaini kukosekana kwa ng'ombe sita baada ya kufanya sensa ya mifugo asubuhi na jioni," alisema Chacha.

Uchunguzi wa awali umebaini uwepo wa wahusika wa upotevu huo miongoni mwa wafanyakazi wa shamba hilo, huku akiahidi kuwa wahusika wote watasakwa, kutiwa mbaroni na kuchukulia hatua za kisheria.

Miongoni mwa wanaoendelea kuchunguzwa ni wanafunzi 60 wa mafunzo atamizi ya ufugaji waliopo kwenye shamba hilo ambao ni kati ya wanaochunga mifugo shambani hapo.

"Mmoja wa waliokamatwa ameonyesha eneo wanapofukia hereni wanazozitoa kutoka kwenye masikio ya ng'ombe waliotoweka. Yupo mtu ambaye ni kinara wa kununua ng'ombe wanaotoweka shamba la mifugo Mabuki....tunamfuatilia na ninaamini tutamtia mbarono karibuni," alisema Chacha.

Meneja wa Chuo cha Ufugaji Kampasi ya Mabuki, Jackob Ngowi alisema shamba hilo lina wanafunzi 60 wanaopata mafunzo atamizi ambapo kila mmoja amekabidhiwa ng'ombe 10 wa kunenepesha.

"Kwa awamu ya kwanza, wanafunzi walinenepesha na kuuza ng'ombe kwa kuingiza faida ya Sh74 milioni," alisema Ngowi.

Pamoja na ufugaji, vijana kupitia mradi wa BBT pia hujifunza mbinu bora za kilimo na ufugaji wa samaki kwenye vizimba.

Kija Masalu, mkazi wa Nhundulu wilayani Misungwi aliiomba Serikali kuimarisha ulinzi wa mifugo na miundombinu ya shamba hilo.